# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

## MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI KITAIFA 1 DESEMBA 2002, IRINGA

**HOTUBA YA MGENI RASMI**
**DR. SALIM AHMED SALIM**

**MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI KITAIFA**

**1 DESEMBA 2002, IRINGA**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa,
Meja Jenerali James Luhanga

Waheshimiwa Mawaziri

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa

Mheshimiwa Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa

Waheshimiwa Viongozi wa Serikali

Waheshimiwa Viongozi wa Dini

Waheshimiwa Madiwani

Waheshimiwa Wageni Waalikwa

Ndugu Wananchi

Kwanza ningependa kuupongeza sana Uongozi wa Mkoa wa Iringa na Wilaya zake kwa kukubali kuchukua jukumu la kuandaa na kufanikisha Maadhimisho haya ya kitaifa ya Siku ya UKIMWI Duniani. Umati ulio mbele yetu unadhihirisha kazi nzuri na kubwa iliyofanyika katika kufanikisha maadhimisho haya. Nawapongeza sana.

Pili, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa kunipa nafasi ya kushiriki katika maadhimisho haya. Kushiriki

kwangu kumenipa nafasi ya pekee ya kuungana na wananchi wa Iringa na wananchi wote wa Tanzania katika harakati za kupambana na hili janga la UKIMWI katika jamii yetu.

Aidha napenda kuwashukuru wakazi wote wa hapa Iringa, ambao ni wenyeji wetu katika maadhimisho haya, na pia WaTanzania kwa ujumla ambao mmejihusisha kwa njia moja au nyingine katika kuipa umihumu siku hii ya leo. Ni imani yangu kwamba kushiriki kwenu katika maadhimisho haya popote pale mlipo ni kielelezo kwamba kila mmoja wetu anaguswa na janga hili la ukimwi na kwamba wote tuna jukumu la kupambana nalo.

Ndugu wananchi, kwa muda mrefu, kwa baadhi yetu, na pengine kwa wengi wetu, iliaminika kwamba ukimwi ni janga lililo mbali nasi binafsi; ambalo linaweza kumpata ndugu mwingine, rafiki au jirani. Ni kweli, tunasikitika na kusononeka tukiwaona wengine, lakini baadae tunasahau. Lakini, katika hali tuliofikia hivi sasa, imejitokeza wazi kwamba dhana hiyo sio sahihi hata kidogo. Wale wenye virusi, wale wenye magonjwa yanayotokana na virusi hivyo, pamoja na wale wasiokuwa navyo, wote tumekuwa waathirika. Ndugu zangu, hali ilivyo hivi sasa, ni kwamba baadhi wameambukizwa lakini wote tumeathirika na janga hili. Hali halisi pia ni kwamba karibu kila mmoja wetu hapa ameguswa; aidha ameuguza au amezika mtoto, mzazi, Ndugu, Jirani, Rafiki au mfanyakazi mwenzake, au ameachiwa watoto yatima.

Kuadhimisha kwetu siku hii ya leo, ni uthibitisho kwamba tunakubali kwamba hili ni janga la jamii yetu yote. Leo, ni siku tunayowakumbuka maelfu ya ndugu zetu tuliowapoteza kwa ugonjwa huu, tunayowakumbuka walio hospitalini na majumbani wakiteseka, na pia malaki wa yatima waliondokewa na wazazi wote, wengi wakiwa na umri mdogo sana.

Pamoja na kuwakumbuka hao wote, leo tunatoa heshima zetu kwa wote wanaowauguza na kuwahudumia wale walioathirika, na pia kutambua wapo miongoni mwetu mamilioni ya Watanzania ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI, na kuwapongeza wale ambao wamekuwa na ujasiri wa kujitangaza na kuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii na kusaidia walioathirika.

Changamoto kubwa zaidi katika maadhimisho haya ni kujizatiti kwetu kama jamii na kwa kila mmoja wetu kuchangia kwa dhati katika kudhibiti ugonjwa huu usisambae zaidi, na katika kuwafanya wenzetu walioathirika waishi maisha ya utu, heshima na faraja zaidi.

Ndugu wananchi, hivi sasa, janga hili duniani limewaambukiza watu karibu milioni 40. Na katika hao walioambukizwa, karibu robo tatu ni Waafrika. Sasa, ikizingatiwa kwamba Waafrika, katika jumla ya idadi ya watu duniani, ni chini ya robo; lakini katika janga la ukimwi sisi tumechukua robo tatu, basi ni dhahiri kuwa hiyo ni hali ya kutisha kwa maisha yetu ya sasa na kwa maendeleo yetu ya baadae.

Hapa nchini, Maelfu ya maelfu ya familia zimeathirika kwa UKIMWI. Tunaambiwa kwamba mkoani Iringa, kama ilivyo kwenye mikoa mingine, idadi ya vifo imeongezeka kiasi kwamba shughuli za mazishi zimekuwa ni matukio ya kila siku katika jamii yetu; mijini na vijijini. Hata hivyo, tunaambiwa kwamba hiki bado sio kilele cha janga hili; kama hatutajizatiti hali itakuwa mbaya zaidi.

Sasa inazidi kudhihirika kwamba UKIMWI ni adui mbaya sana kwa jamii na taifa kwa ujumla. Ni adui mbaya ambaye anaingia kwenye nyumba zetu kimya kimya. Anatulia na kutafuna wanafamilia pole pole na kimya kimya kwa miaka mitano hadi kumi, na hatimaye kuwatoa roho wanafamilia mmoja baada ya mwingine. UKIMWI unatumalizia wazazi wetu, unatumalizia watoto wetu, unatumalizia ndugu zetu, rafiki zetu na wafanyakazi wenzetu.

Ndugu wananchi, kwa miaka mingi bara letu hili la Africa limehusishwa na vita na maafa ya kutokana na migogoro. Tumepoteza watu wengi sana katika vita za migogoro ya aina hiyo. Lakini, hadi kufikia sasa, imebainika kwamba ukichanganya idadi ya watu waliopoteza roho katika vita vyote vilivyopigana Afrika tokea nchi zetu zipate uhuru, pamoja na migogoro ya muda mrefu kama ya Angola, Sudan, Somalia na kwingineko, bado idadi ya watu tuliopoteza kutokana na migogoro hiyo ni ndogo ikifananishwa na ile ya waliofariki kutoka na janga la ukwimi.

Mbaya zaidi, ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya wanaoambukizwa virusi, kuugua UKIMWI na kufariki ni watu wenye umri kati ya miaka 20 – 49 na hasa vijana. Kundi hili ndilo linalotegemewa na familia na taifa kwa ujumla katika utendaji na uzalishaji mali. Pamoja na kukosesha familia na taifa nguvu kazi, idadi kubwa ya vifo katika kundi hii husababisha ufukara na ongezeko kubwa la watoto yatima katika familia zetu. Yatima ambao wanabakia kulelewa na bibi na babu au ndugu wengine ambao pia hawana uwezo na ambao wenyewe wanategemea msaada.

Hivyo, leo ni siku ya kila mmoja wetu kutafakari kwa makini na kujiuliza; Je huyu adui UKIMWI atatufikisha wapi? Je, tutamwachia aendelee kutumaliza? Je tufanye nini kupunguza ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika jamii yetu.

Jambo la kusikitisha na kuogopesha ni kwamba pamoja na kwamba tunauelewa ugonjwa wa UKIMWI na jinsi unavyoambukizwa, kiwango cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI kinaendelea kuongezeka kwa kasi kila siku katika jamii yetu. Hii inadhihirisha wazi kwamba bado sisi jamii ya Watanzania hatujawa makini katika kudhibiti UKIMWI.

Ni dhahiri kwamba bado tunachukulia suala la UKIMWI kimzaha mzaha tu. Hii ni hatari sana kwa maisha yetu na taifa letu. Tunachukulia kimzaha adui UKIMWI anayetumaliza. Ni muhimu sana tuuone UKIMWI uliopo kati yetu sisi tunaofikiri tu salama, kuliko kuuona UKIMWI kwa walioathirika na wagonjwa. Tuuone UKIMWI

umejificha katika maisha yetu ya kila siku, katika familia zetu, katika sehemu zetu za kazi, katika shule zetu, katika sehemu zetu za burudani na vilabu vyetu. Tuuone na tuwe na mikakati thabiti ya uhakika ya kuudhibiti.

Ndugu Wananchi, ukimwi hauchagui kabila, hauchagui dini, hauchagui rangi, hauchagui masikini wala tajiri, mzee au kijana. Hili ni janga linaemkuta yoyote yule asiepuka kuambukizwa na asietumia kinga. Iko haja ya sote, mmoja mmoja na kwa pamoja kuchukua hatua madhubuti kujinusuru wenyewe na kunusuru jamii yetu na vizazi vyetu vijavyo. Yapo matumaini kwamba pale jamii inapojizatiti na kuchukua hatua madhubuti, matokeo yamekuwa ya kutia moyo katika kudhibiti janga hili.

Kwa bahati mbaya sana Watanzania tumejenga tabia ya kutokujadili kwa uwazi changamoto na mikakati ya uhakika ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Ukimya, usiri na hali ya kujificha tunayoijenga ni msingi wa maangamizi yetu. Janga hili tunalo na haisaidii kukataa kwamba lipo. Inabidi tulikabili ana kwa ana kwa kulizungumzia kinaganaga kwa jinsi lilivyotuathiri na jinsi ya kupambana nalo. Haisadii, kubaki tunaonyesheana vidole na kungojea tu mpaka watoto wetu, wazazi wetu, ndugu zetu na wafanyakazi wenzetu waugue, wafe na tuwazike. Tunakaa kimya tu na huku huyu adui UKIMWI anazidi kujizatiti katika familia zetu na kutumaliza. Tutakaa kimya mpaka lini? Mpaka tuishe wote?

Tunaelewa wazi kwamba zaidi ya asilimia 90 ya maambukizi ya virus vya UKIMWI yanatokana na kujamiiana. Lakini bado hatujashtuka. Bado hatujabadilika katika tabia zetu za kujamiiana. Bado hatujawa makini na kutambua ukweli kwamba tendo la kujamiiana linaweza kuwa ndiyo mwanzo wa **UKIMWI.** Maandiko matakatifu yanatuasa na kukataza zinaa. Bado tunafanya mzaha. Wale waliosoma vitabu vitakatifu watakumbuka waliyoyapata watu wa Sodoma na Gomora.

Pia ni muhimu tukumbuke kwamba pamoja na jitihada za watafiti duniani kote, mpaka sasa hakuna chanjo wala tiba ya UKIMWI. Dawa zilizopo ikiwa ni pamoja na dawa za jadi zinasaidia kumpa mgonjwa ahaueni tu. Hivyo, tumaini letu la kujikinga na janga hili la UKIMWI ni kuhakikisha kwamba hatuambukizwi virusi vya UKIMWI. Na hili linawezekana kabisa. Ni jukumu la kila mmoja wetu ajali afya yake kwa kutokuambukizwa Virusi vya UKIMWI. Ndiyo maana ujumbe wa mwaka jana wa Siku ya UKIMWI duniani ulikuwa - **"MIMI NAJALI WEWE JE".** Huu ni ujumbe mzito ambao kila mmoja wetu anahitaji kuuzingatia kila siku katika maisha yetu. Ujumbe huu unasisitiza kwamba:

- Kwanza ujali maisha na afya yako. Hivyo uchukue kila tahadhari kuhakikisha kwamba huambukizwi virusi vya UKIMWI.
- Pili kama unajali maisha na afya yako, mhimize pia mwenzio naye ajali maisha na afya yake kwa kutokuambukizwa Virusi vya UKIMWI.

- Tatu kama unajali maisha na afya yako, nenda kapime damu yako ili ujihakikishie hali ya afya yako. Kama huna virusi, kama inavyoaminika kwamba zaidi ya asilimia 85 ya watu wazima hawana virusi vya UKIMWI, itakupa hamasa kubwa ya kuendelea kujali na kujilinda. Iwapo mtu atajigundua kwamba ana virusi, basi ana nafasi nzuri ya kupata ushauri nasaha mapema jinsi ya kujitunza na kuendelea na maisha kama kawaida kwa miaka na miaka kuliko kungojea mpaka anaanza kupata dalili za ugonjwa huu. Tusiogope kupima afya zetu.
- Nne, ujumbe huu unatuasa kwamba, tufikiri mara mbili kabla ya kufanya tendo la kujamiiana; kila mmoja atafakari tena Maisha na Afya yake na usalama wa tendo lenyewe.

Ujumbe wa mwaka huu ni: **'UKIMWI HAUBAGUI, SISI TUNABAGUA'** Ujumbe huu unendeleza na kusisitiza Ujumbe wa mwaka jana. Pamoja na kujilinda, sasa tuache ubaguzi na unyenyepa kwa wale wote walioathirika na janga hili. Hawa ni pamoja na wenzetu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na watoto yatima ambao wamepoteza wazazi wao kutokana na janga hili. Kama wenzetu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI walivyotueleza hapa kwamba ni muhimu tukumbuke kwamba UKIMWI ni ugonjwa kama magonjwa mengine. Hivyo, tuache kabisa tabia ya kuwahukumu na kuwaona kama wao ni wenye dhambi. Tuache unafiki wa kujiona kwamba sisi tu bora zaidi kuliko wale wenzetu wenye Virusi vya UKIMWI au watoto yatima.

Aidha, tusijisahau nafsi zetu. Tunapowabagua na kuwafedhehesha wenzetu wenye kuishi na Virusi vya UKIMWI, tunajibagua na kujifedhehesha sisi wenyewe kwa sababu labda siku moja sisi wenyewe, au ndugu zetu, au watoto wetu tutajikuta tuna virusi vya UKIMWI. Ninapenda kuchukua nafasi hii kuungana na wale wote wanaokemea tabia ya baadhi ya watu wanaowabagua na kuwafedhehesha wenzetu wenye kuishi na Virusi vya UKIMWI, na badala yake tuwaonyeshe upendo na tuwasaidie na kuwahudumia kadri ya uwezo wetu.

Katika kukabiliana na janga hili, ni lazima kila mmoja wetu ajihusishe kikamilifu katika harakati za kudhibiti UKIMWI. Kila mmoja wetu atafakari mwenendo wake kimaisha, tujadili kwa uwazi kabisa katika familia, vijiji, jumuiya, sehemu za kazi jinsi ya kijikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na jinsi ya kuwahudumia wenzetu walioathirika na virusi, wagonjwa na yatima, katika jamii zetu.

Katika bara letu la Afrika na katika nchi yetu tunapaswa kutambua kwamba tumo katika vita. Na ni dhahiri kuwa katika vita vyovyote vile tunapaswa kuhakikisha kwamba taifa lote limejiandaa kikamilifu kumshinda adui anayevamia nchi.

Kwa mfano sote tunakumbuka kwamba wakati nduli Iddi Amini alipovamia mipaka yetu na kuteka sehemu moja ya nchi yetu, taifa letu na jamii yetu yote iliamka kwa ujasiri na kila mmoja wetu alikuwa tayari kutoa mchango wake kutetea watu wetu na nchi yetu.

Tulikusanyika kama majeshi ya ulinzi, mgambo na kadhalika na tukaelekeza silaha zetu na nyenzo zetu zote za kiuchumi na kisiasa katika kukabiliana na tishio hilo kwa Taifa letu.

Janga la ukimwi ni tishio kubwa zaidi. WaTanzania wengi zaidi wameuawa na mvamizi huyu – ukimwi. Hali ya uchumi wetu inaathirika vibaya zaidi kutokana na adui huyu ukimwi, maisha yetu na ya vizazi vijavyo yako mashakani kutokana na janga hili. Ukimwi ni tishio la usalama wa Taifa.

Ndugu wananchi tumevamiwa na tunaangamia. Tukifanya mchezo tutateketea. Tunapoteza wananchi wetu, tunakwamishwa maendeleo yetu, na tunaelekeza rasilimali zetu katika maeneo tusiotarajia. Hivi ni vita, na iko haja ya kujibu mapigo.

Tunapaswa kuingia katika hali ya mapambano ya kivita dhidi ya adui huyu. Kila mmoja wetu anapaswa kutoa mchango wake kumkabili adui ili kujilinda sisi wenyewe na kuokoa vizazi vijavyo, na kunusuru taifa hili. Safari hii mapambano haya sio ya kijeshi kwa sababu adui ameshaingia majumbani mwetu na kafika hadi vitandani mwetu. Hatuna budi kumng'oa.

Hili sio pambano la sekta moja. Sio la mahospitali peke yao, sio la waganga wa jadi pekee, sio la misikitini na kanisani, shuleni au makazini tu. Hili ni pambano la kila mahala. Tupange safu zetu na kutii amri za majemadari wetu ili tupate ushindi.

Hivi ni vita ambavyo lazima tushinde. Vinginevyo tutateketea kama jamii na kama Taifa. Hatuwezi kukubali hilo. Ndio maana kila mmoja wetu anawajibika kutoa mchango wake. Siku hii ya leo ambapo sisi Watanzania na wenzetu kote duniani wanaitumia kutafakari na kujikumbusha juu ya janga kubwa la ukimwi ni siku muwafaka ya kuimarisha nia zetu na kujizatiti zaidi katika kupambana na adui huyu.

Ahsante sana kwa kunisikilza.